

13B-Aina Za Al-Waqf (Kisimamo) Na Sababu Zake

Aina Za **الْوَقْفُ** Al-Waqf - Kisimamo Na Sababu Zake:

Kusimama hutokea kutokana na moja kati ya sababu nne zifuatazo:

KWANZA: **الْوَقْفُ الإِضْطِرَّارِي Al-Waqf Al-Idhwtwiraariy - Kisimamao Cha Dharura**

Msomaji hulazimika kusimama kutokana na kuishiwa pumzi au kikohozi, kupiga chafya, au kusahau n.k. nako kunajuzu kusimama juu ya neno lolote. Ikiwa ni mahali pa kuruhusiwa atarudi kusoma kuanzia lile neno alilosimamia. Ikiwa ni mahali pasiporuhusiwa atarudi nyuma kidogo kuanza maneno yatakayoleta maana.

PILI: **الْوَقْفُ الإِخْتِيَارِي Al-Waqf Al-Ikhtibaariy - Kisimamo Cha Mtihani:**

Kisimamo anachosimamishwa mwanafunzi na mwalimu wakati wa kufunzwa au kufanyiwa mtihani, ikiwa ni kumtanabahisha kosa au kumjulisha amemaliza mtihani wake.

TATU: **الْوَقْفُ الإِنْتِظَارِي Al-Waqf Al-Intidhwaariy - Kisimamo Cha Kusubiri**


Kisimamo kinachotumika kwa *Mutakhasw-swiswuwn* (watu walioshughulika zaidi) katika fani ya *qiraa-ah* zaidi ya kimoja na husimama kwa ajili ya kubadilisha aina ya *qiraa-ah* kimoja na kusoma *qiraa-ah* chengine.

NNE: **الْوَقْفُ الإِخْتِيَارِي Al-Waqf Al-Ikhtiyaariy - Kisimamo Cha Hiari**

Kisimamo ambacho msomaji hukusudia kusimama kwa uchaguzi wake au hiari yake mwenyewe. Kisimamo hiki cha hiari ndio chenye hukmu katika usomaji wa Qur-aan; nacho kimegawanyika sehemu mbili:

الجائز Al-Jaaiz - Kinachofaa: kimegawanyika sehemu tatu.

غير جائز Ghayru Jaaiz - Kisichofaa: Ni kimoja tu.



Visimamo vyote vya الجائز (Al-Jaaiz) ni vyenye kutimiza maana katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) ila zimetofautiana kwa daraja za ubora; kuanzia kilicho bora kabisa ni التام (At-Taamm), kisha kinachofuatia kwa ubora ni الكافي (Al-Kaafi), na mwishowe ni kisimamo cha الحسن (Al-Hasan). Tafauti hizi ni kwa sababu ya kimaana na kilugha¹

¹ Rejea Mlango wa 'Alama Za Kusimama Katika Msahafu' ambao imebainishwa uhusiano huo.